# USAFIRISHAJI WA MIFUGO NA MAZAO YAKE NDANI NA NJE YA NCHI

## A. UTARATIBU WA KUSAFIRISHA MIFUGO NDANI YA NCHI

Usafirishaji wa mifugo/wanyama ndani ya nchi hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama sura 159 kupitia Kanuni zake za Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na Mazao ya Wanyama ya Mwaka 2007 ikisomwa Pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2020 (**GN 489A tarehe 29 Juni, 2020**). Lengo kuu la Kanuni hii ni kudhibiti usambaaji wa magonjwa ya mifugo ya Wanyama hivyo kulinda uchumi wa wafugaji na taifa kwa ujumla na pia kulinda afya ya Jamii dhidi ya magonjwa au madhara yanayoweza kuwapata binadamu kutokana na mifugo/Wanyama.

Kuna aina mbili za wadau wa usafirishaji mifugo ndani ya nchi. Aina hizo za Wadau wa Mifugo ni wale wenye Mifugo inayosafirishwa kwa ajili ya Biashara na wale wenye Mifugo inayosafirishwa kwa ajili ya kwenda kufugwa eneo jingine ndani ya nchi.

### 1. Mifugo inayosafirishwa kwa ajili ya Biashara

Ili kuweza kusafirisha mifugo ndani ya nchi kwa ajili ya biashara, Mfanyabiashara anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe na nambari ya mlipakodi ya Mamlaka ya mapato Tanzani (TRA) pamoja na *Tax clearance.*

(b) Awe amesajiliwa na anatambuliwa na Bodi ya Nyama Tanzania (Tanzania Meat Board-TMB)

(c) Awe na leseni ya biashara ya kusafirisha mifugo ndani ya nchi ambayo hutolewa na Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia BRELA. Mfanyabiashara atatakiwa kuomba leseni hii kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya BRELA ambayo ni https://ors.brela.go.tz akiambatisha na nyaraka zilizotajwa hapo juu pamoja na barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Minada wa mojawapo ya minada ya upili nchini.

(d) Mfanyabiashara mwenye nyaraka zilizotajwa hapo juu atatakiwa kulipia gharama za ukaguzi na kukata kibali cha kusafirisha mifugo/Wanyama (*Animal Health Livestock Movement Permit*) kila safari ya kusafirisha wanyama. Kibali hiki hupatikana kwa Wakaguzi wa Mifugo walioko minadani, Kwenye Ofisi za Idara ya Mifugo katika Halmashauri za Serikali za Mitaa zote nchini au kwa Afisa Mifugo wa Serikali aliyekasimishwa

madaraka na Daktari wa Mifugo wa Wilaya (DVO) kutunza na kutoa nyaraka hizo.

Gharama za kusafirisha aina mbalimbali za mifugo ndani ya nchi zimeainishwa kwenye jedwali No. 1

**2. Mifugo Inayosafirishwa kwa Ajili ya kufugwa**

Mtu yeyote anayetaka kusafirisha mifugo (isipokuwa ndege wafugwao) atatakiwa:

(a) Kuwa na barua au uthibitisho kutoka Serikali za Mitaa za Kijiji/mtaa na kupitishwa na Daktari au Mkuu wa Idara ya Mifugo katika Halmashauri za Serikali za Mitaa.

(b) kulipia gharama za ukaguzi na kukata na kibali cha kusafirisha mifugo/Wanyama (*Animal Health Livestock Movement Permit*) kila safari (*consignment*). Kibali hiki hupatikana kwa Wakaguzi wa Mifugo walioko minadani, Kwenye Ofisi za Idara ya Mifugo katika Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kote nchini au kwa Afisa Mifugo wa Serikali aliyekasimishwa madaraka kutunza na kutoa nyaraka hizo.

**3. Tozo za vibali vya kusafirisha Mifugo ndani ya Nchi**

Gharama za kusafirisha aina mbalimbali za mifugo ndani ya nchi kwa mujibu wa GN 489A zimeainishwa kwenye jedwali No. 1 hapa chini.

**Jedwali Na. 1**

| S/N | Aina ya Mnyama au bidha | Kipimo kinacholipiwa *(Unit)* | Kiwangocha tozo (Shs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng’ombe | Kila mmoja | 2,500 |
| 2. | Mbuzi /Kondoo | Kila mmoja | 1,500 |
| 3. | Punda/ Farasi/Mule | Kila mmoja | 2,500 |
| 4. | Mbwa/Paka | Kila mmoja | 1,000 |
| 5. | nguruwe | Kila mmoja | 1,500 |

| S/N | Aina ya Mnyama au bidha | Kipimo kinacholipiwa *(Unit)* | Kiwangocha tozo (Shs) |
|---|---|---|---|
| 6. | ngamia | Kila mmoja | 2,500 |
| 7. | Mayai aina zote chini ya trei 100 | trei | 0 |
| 8. | Mayai ya kula Zaidi ya trei 100 | trei | 200 |
| 9. | Mayai ya kutotolesha Zaidi ya trei 100 | trei | 500 |
| 10 | Wanyamapori | Kila mmoja | 1,000 |
| 11 | ndegepori | Kila mmoja | 500 |
| 12 | Ngozi ya za ng'ombe, punda na farasi | Kibali | 1,000 |
| 13 | Ngozi za mbuzi na kondoo | Kibali | 0 |
| 14 | mbolea | Tani | 1,000 |
| 15 | Pembe, Kwato, mifupa na vitu vingine vitokanavyo na mabaki ya mbuzi, ng'ombe, kondoo na aina zote za mifugo | Kibali | 20,0000 |
| 16 | Chakula cha mifugo | Kibali | 5,000 |

## B: UTARATIBU WA KUAGIZA MIFUGO NA MAZAO YA MIFUGO KUTOKA NA KUINGIA NDANI YA NCHI

Uagizaji na Usafirishaji Mifugo/wanyama na Mazo ya mifugo nje ya nchi hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama sura 159 kupitia Kanuni zake za Udhibiti wa Usafirishaji wa Wanyama na Mazao ya Wanyama ya Mwaka 2007 ikisomwa Pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2020 (**GN 489A tarehe 29 Juni, 2020**). Gharama za bidhaa au Wanyama anazopaswa kutozwa mteja kwa kipindi hiki kuanzia Julai 2020 zimetajwa kwenye majedwali yaliyoko ndani ya Kanuni hizo (GN 489A) ambazo pia zinapatikana kwenye tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Utaratibu wa Kuomba vibali vya kuagiza mifugo/mazao ya mifugo kutoka na kuingia Tanzania ni kama ifuatavyo:

i. Ingia kwenye tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa anuani: www.mifugouvuvi.go.tz upakue fomu ya maombi kulingana na hitaji lako. Katika tovuti kuna fomu zifuatazo: Fomu ya kuomba kibali cha Kuagiza Mazao ya Mifugo au vyakula vyamifogo kutoka nje ya nchi (IMPORTATION APPLICATION FORM FOR ANIMAL PRODUCTS AND ANIMAL FEEDS
ii. Fomu ya kuomba kibali cha kuagiza Wanyama toka nje ya nchi (IMPORTATION APPLICATION FORM FOR ANIMALS)
iii. Fomu ya kuomba kibali cha kusafirisha Wanyama kwenda nje ya nchim (APPLICATION FORM FOR EXPORT PERMIT (INTERNATIONAL HEALTH CERTIFICATE) FOR ANIMALS)
iv. Fomu ya kuomba kusajiliwa kama wakala au kufanya biashara ya vifaranga na Mayai totoleshi (APPLICATION FORM FOR REGISTRATION OF DEALERS, AGENTS AND BROKERS OF DAY OLD CHICKS AND HATCHING EGGS)
v. Fomu ya kuomba kibali cha kusafirisha ndege porin je ya nchi (APPLICATION FORM FOR EXPORT PERMIT (INTERNATIONAL HEALTH CERTIFICATE) FOR LIVE WILD BIRDS)
vi. Fomu ya kuomba kibali cha kuanzisha vitotoleshi (APPLICATION FORM FOR THE ESTABLISHMENT OF A HATCHERY OR BREEDER FLOCK FARM)
vii. Fomu ya kuomba kusajili Machinjio (APPLICATION FORM FOR REGISTRATION OF A SLAUGHTER FACILITY)
viii. Fomu ya kuomba kibali cha kusafirisha bidhaa za ziada za mfugo nje ya nchi (APPLICATION FORM FOR EXPORT PERMIT (INTERNATIONAL HEALTH CERTIFICATE) FOR ANIMAL BY-PRODUCTS
ix. Fomu ya kuomba kibali cha kusafirisha nyama na mazao ya nyama nje ya nchi (APPLICATION FORM FOR EXPORT PERMIT (INTERNATIONAL HEALTH CERTIFICATE) FOR MEAT AND MEAT PRODUCTS)

17. Ukishachagua fomu husika na kuijaza itume kupitia anuani ya barua pepe ya Masijala ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambayo ni barua@mifugo.go.tz; au zvc.arusha@mifugo.go.tz, naic@mifugo.go.tz, kama upo mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Arusha au Manyara; zvc.mwanza@mifugo.go.tz, mabuki@mifugo.go.tz kama

upo Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Mara au Simiyu; zvc.tabora@mifugo.go.tz kama upo mikoa ya Tabora au Kigoma; zvc.sumbawaga@mifugo.go.tz kama upo mikoa ya Katavi au Rukwa; zvc.iringa@mifugo.go.tz, saohill@mifugo.go.tz, kitulo@mifugo.go.tz, langwira@mifugo.go.tz kama upo mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe, Ruvuma au Songwe. Barua pepe nyingine ni ngerengere@mifugo.go.tz, zvc.temeke@mifugo.go.tz, vikuge@mifugo.go.tz kama upo mikoa ya Dar es Salaam, Pwani au Morogoro; zvc.mtwara@mifugo.go.tz, nangaramo@mifugo.go.tz kama upo mikoa ya Mtwara au Lindi na zvc.dodoma@mifugo.go.tz kama upo Mikoa ya Dodoma au Singida.

18. Unapotuma fomu iliyojazwa ambatisha nyaraka zote kama zilivyotajwa kwenye fomu husika.
19. Maombi yako yakishafika Wizarani utatayarishiwa Akara ya malipo na utatumiwa control number kupitia simu yako uliyoijaza kwenye fomu.
20. Ukishalipa na kutuma *bank pay in slip* utatayarishiwa kibali.